



NY State of Health Huwaunganisha Wakazi wa New York na Bima za Afya Zenye Bei Nafuu

Huwa tunakusaidia kulinganisha mipango ya afya na kupata chaguo bora kwa ajili yako na familia yako.

NY State of Health hukupa mipango ya bila malipo au ya bei nafuu, huduma za uzuiaji zisizolipishwa, mipango isiyo na malipo ya kulipa mwenyewe kwa ajili ya huduma za msingi na dawa za bei nafuu. Usaidizi wa kifedha ulioongezwa wa serikali kuu unapatikana ili kupunguza gharama za bima ya afya kwa wakazi zaidi wa New York.

MIPANGO INAJUMUISHA:

- 1 Medicaid
- 2 Child Health Plus
- 3 Essential Plan
- 4 Qualified Health Plans

Unapojiandikisha, tayarisha taarifa hizi za kila jamaa wa familia yako:

- ✓ Tarehe za kuzaliwa
- ✓ Nambari za usalama wa jamii au, kwa wahamiaji halali, nambari za stakabadhi ikiwa zipo
- ✓ Taarifa za uajiri, mapato na taarifa za bima za afya zinazofadhiliwa na mwajiri

Wasiliana nasi ili ujiandikishe au upate maelezo zaidi:

- Tembelea nystateofhealth.ny.gov
- Piga simu kwa 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220)
- Pata usaidizi bila malipo kutoka kwa msaidizi wa kujiandikisha. Unaweza kumpata katika <https://info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor>

Taarifa kwa Wanaojiandikisha

Ikiwa umejiandisha katika bima ya afya kupitia NY State of Health, endelea kufuatilia ili usikose taarifa muhimu, ikiwa ni pamoja na wakati wa kusasisha mpango wako wa bima.

1 Jisajili ili upokee arifa kwa njia ya SMS.

Ili Ujisajili, tuma ujumbe wenye neno START kwa 1-866-988-0327

2 Sasisha taarifa za akaunti yako.

Hakikisha kuwa NY State of Health ina maelezo unayotumia sasa ya anwani ya posta, nambari ya simu na anwani ya barua pepe ili tuweze kuwasiliana nawe kuhusu bima yako ya afya.

- Piga simu kwa 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220)
- Ingia katika akaunti yako kupitia nystateofhealth.ny.gov
- Wasiliana na msaidizi wa kujiandikisha. Unaweza kumpata katika <https://info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor/>

3 Ukipata habari kutoka kwa NY State of Health, ni wakati wa kuchukua hatua kwenye bima yako ya afya.

Angalia kikasha chako cha barua pepe na cha barua za posta ili uone kama kuna taarifa na ilani muhimu. Fuata maagizo na usasishe mpango wako wa bima kabla ya tarehe ya mwisho iliyotolewa.

TUPO HAPA KUSAIDIA!

WASILIANA NASI IWAPO UNA MASWALI.